**OFISI YA RAISI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**SHULE YA SEKONDARI NKEREGE**
**S. L. P 233, TARIME**

---

Jina La Mzazi/Mlezi ...............................................................................................

shule ya msingi ...............................................................................................

**YAH:- MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021**

ninafuraha kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari nkerege, kidato cha kwanza mwaka 2021

1. **MAELEKEZO**

❖ Shule ya sekondari nkerege ni ya mchangamano (wavulana na wasichana), shule ipo katika kijiji cha nkerege kata ya kiore wilaya ya tarime.
❖ Ni matumaini yangu kuwa mwanao ataitumia nafasi hii vizuri kujifunza kwa bidii ndani na nje ya darasa wakati wote awapo shuleni.
❖ Ni wajibu wako mzazi/mlezi kuhakikisha mwanao unampatia maadili, wosia na mahitaji yote kabla hajafika hapa shuleni asije akapoteza nafasi hii muhimu aliyopewa.
❖ Unatakiwa kupata taarifa ya maendeleo ya mwanao kitabia na kimasomo kila muhula.
❖ Unatakiwa kumpatia mwanao mahitaji muhimu ya kila siku kama vile malazi, chakula, mavazi na mengineyo.
❖ Kama upo mbali na shule mzazi/mlezi utalazimika kumtafutia mwano mahali pa kuishi pamoja na uangalizi kimalezi awapo kwenye pango lake baada ya saa za masomo.
❖ Mzazi/mlezi utawajibika kutembea na kupata taarifa kwa mwenye nyumba alipopanga mwanao ili kupunguza uhuru, tabia mbaya ya utoro usio na msingi, mambo ya mapenzi, uvutaji sigara na utumiaji wa madawa ya kulevya na unywaji wa pombe.

2. Kulipoti shuleni
   Shule itafunguliwa mnamo tarehe11/01/2021. Mwanao anatakiwa kulipoti siku hiyo shuleni mwanafunzi ataripoti ndani ya siku saba (7)

3. **SARE YA SHULE**
   a. Skieti mbili (2) zote nyeusi ziwe ndefu zinazofunika soksi, kitambaa kizito sio kisukarikisukari, kwa wasichana tu.
   b. Suruari mbili (2) zote nyeusi, zenye mjarinda mawili (2), zisiwe za kuvalia kwenye matako kwa stahili za kata “k” na zisiwe mdol kwa wavulana.
   c. Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi kwa wavulana na wasichana
   d. Soksi nyeupe jozi (2) kwa wasichana.
   e. Truck suit nyeupe na raba kwa wavulana na wasichana kwa ajiri ya michezo.
   f. Sweta la blue lenye shingo “v”.
   g. Tai mbili (2) nyeusi

h. Mkanda mweusi sio usio na mapambo wala urembo wowote (kwa wavulana).
i. Soksi nyeusi jozi mbili (2) kwa wavulana.

Maagizo ya kuzingatia katika uvaaji na usafi wa mwanafunzi.

- Wakati wote shati lazima liwe limechomekwa na vishikizo vya shati vifungwe.
- Hairuhusiwi kutumia vipodozi (angle face, plastic, deep face, wanja n.k) akiwa shuleni.
- Hairuhusiwi kuvaa heleni, pete, bangili, kupaka kucha rangi na mapambo ya aina yoyote.
- Nywele ziwe fupi, hairuhusiwi kunyoa mitindo kama vile kiduku, funky, kupaka madawa kama vile carl, raster, golden hair, wave n.k.
- Hairuhusiwi kufuga ndevu wala kuvaa kofia akiwa shuleni.
- Viatu vya wazi (openi shooes) yeboyebo, bajaj, na ndala ni marufuku shuleni.

**4. <u>VIFAA</u>**

Mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo:-

a. Madaftari makubwa kumi (10) counter books.
b. Vifaa vya hesabu (mathematical set).
c. Kalamu za wino, pensel na rula.
d. Dictionary (English – English) kwa ajili ya matumizi yako.
e. Begi la kubebea madaftari / vitabu mifuko ya karatasi :(pepsi ni marufuku.)
f. Ream paper A4(1)
g. File (1)
h. Fyekeo kwa ajili ya usafi wa mazingira kwa wavulana na wasichana
i. Madaftari madogo kumi (10) msomi
j. Graph pad (1), passport size (4)

**5. <u>FOMU MAALUMU YA MATIBABU.</u>**

Fomu ijazwe na mganga wa hospitali ya wilaya/kituo cha afya kinachotambulika na serikali na siyo mganga wa zahanati. (iletwe shuleni siku ya kuripoti)

6. **<u>SHERIA ZA SHULE</u>**.

Sheria za shule zimeambatanishwa, mwanafunzi anatakiwa azisome kwa makini na mwisho asaini katika fomu iliyoambatanishwa ili kuonyesha kukubaliana na sheria hizo.

**7. <u>CHETI CHA KUZALIWA.</u>**

Mwanafunzi anatakiwa alete nakala ya cheti cha kuzaliwa (photocopy) siku ya kuripoti shuleni.

*EMAKULATA L. MAPUNDA*
*contact no: 0742 322 044*

# SHERIA ZA SHULE

Sheria hizi zinalenga kukupa **UTII, HESHIMA na NIDHAMU.**

1. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu, mtu yeyote au kundi la watu wanaomzidi umri popote awaonapo au kukutana nao.
2. Ni marufuku kutumia lugha chafu wakati wowote kwa walimu wao, wao kwa wao na watu wengine.
3. Unatakiwa kuheshimu alama za taifa. Mfano bendera ya taifa, viongozi wa taifa na nembo ya taifa na wimbo wa taifa.
4. Hauruhusiwi kuonekana au kutembelea:-
   (a) vilabu vya pombe.
   (b) kumbi za starehe.
   (c) nyumba za kulala wageni.
   (d) nyumba za walimu/watumishi bila ruhusa.
5. Huruhusiwi kuharibu mali za shule.
6. Ni muhimu kuzingatia usafi binafsi na kuhifadhi mazingira ya shule.
7. Huruhusiwi kupiga kelele ovyo ndani na nje ya madarasa.
8. Unatakiwa kutumia kiingereza wakati wote ndani na nje ya madarasa.
9. Ni marufuku kabisa kwa wanafunzi:-
   (a) kuvuta sigara, kuja darasani ukiwa umelewa au kuja shuleni na kilevi cha aina yeyote. Mfano bangi, viroba n.k.
   (b) kufuga kucha na kuzipaka rangi.
   (c) kufuga ndevu na nywere ndefu.
   (d) kuvaa mavazi yasiyo na heshima.
   (e) kugombana ama kupigana.
   (f) kutoroka darasani au kazini.
   (g) kuvaa kofia au bangili na mapambo mengine yasiyo ya lazima.
   (h) kuiga mitindo ya kihuni. Mfano mavazi, kunyoa kipara n.k.
   (i) kuchubua ngozi ya mwili kwa kutumia madawa.
10. Unatakiwa kuhudhuria vipindi vyote darasani na kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote inayotolewa na mwalimu.
11. Huruhusiwi kwenda nje ya shule bila ruhusa wakati wa vipindi.
12. Ni lazima kuvaa sare ya shule kila uwapo katika eneo la shule.
13. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu shuleni na nje ya shule.

# TARIME DISTRICT COUNCIL

## Nkerege Secondary School
## P. O. BOX 233, Tarime

## MEDICAL EXAMINATION FORM

Full name:
..........................................................................................................................
Age: ........................ Height (in cms)................... Weight................

1. Blood count: ..................................... red and white .................................
2. Stool examination: .........................................................................................
3. Urinalysis: ...........................................................................................................
4. Syphilis and other V.D: ..........................................................................
5. T.B and leapers test: ..............................................................................
6. Eye test: ..............................................................................................
7. Ear test: ..............................................................................................
8. Chest test: ..........................................................................................
9. Plano test (girls): ........................................................................................
10. Spleen: ..........................................................................................................

Addition information, eg. Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseas (eg. Sickle cell), inability to eat certain food etc.

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................

I certify that the above named student is fit/is not fit to pursue Secondary Education.

Date: ................./............/20.....

Signature: ..........................................................

Destination: ..........................................................

Station: ...................................................................